TANGAZO LA SERIKALI Na. 1029 la tarehe 11/12/2020

(SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO ZA UANZISHAJI WA VIKUNDI VYA WATUMIAJI WA MAJI ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Uanzishaji wa Vikundi vya Watumiaji wa Maji za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama za Mwaka 2020.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo;-

"Afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"chanzo cha Maji" maana yake ni kisima kilichoboreshwa na chenye mzingo wa mita 60;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama;

"Halmashauri ya Kijiji" maana yake ni Halmashauri ya Kijiji ambacho chanzo cha maji kimo;

"Kijiji" maana yake ni Kijiji ambamo chanzo cha maji kimo;

"Kikundi cha Watumiaji wa Maji" maana yake ni muungano wa watu unaomiliki huduma ya maji na unaoundwa na watu binafsi au kaya zinazochota maji kwenye chanzo cha maji na ambao wamejiunga kwa hiari kuanzisha na kuendeleza huduma ya maji na usafi wa mazingira katika Kijiji au Kitongoji na ambacho kimesajiliwa kisheria na Halmashauri na inajumuisha Taasisi au Jumuiya zinazotambulika kisheria;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Mkalama.

Cheti cha umiliki wa eneo la chanzo cha maji

4.-(1) Halmashauri itatoa cheti cha umiliki wa eneo la chanzo cha maji kwa Kikundi cha Watumiaji wa maji kilichopo katika eneo la Halmashauri.

Wajibu wa Kikundi

5. Kikundi cha Watumiaji wa Maji kitakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kutunza mazingira ya chanzo cha maji;

(b) kuhakikisha ulinzi na usalama wa chanzo cha maji; na

(c) kurejesha pampu na vifaa vingine endapo vitaharibika au kuibiwa.

Wajibu wa Halmashauri ya kijiji

6. Halmashauri ya Kijiji itakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kutoa ushauri, kuhamasisha, kuunga mkono, kulinda na kusimamia vikundi vya watumiaji maji vilivyo katika eneo lake;

(b) kupokea na kuidhinisha mkataba wa makubaliano ya watumiaji wa maji na kuhakikisha kuwa yanatekelezwa ipasavyo;

(c) kutoa taarifa ya maandishi kwa Mkurugenzi kuhusu migogoro itakayojitokeza miongoni mwa watumiaji wa maji au kati ya watumiaji wa maji na Halmashauri ya Kijiji kwa ajili ya uamuzi wa Mkurugenzi.

Uwezo wa kukagua

7. Afisa mwidhiniwa anaweza, katika muda wa kazi, kuingia kwenye chanzo cha maji kwa lengo la kukagua na kuhakikisha kuwa Kikundi cha Watumiaji wa Maji kinaendesha shughuli zake kwa mujibu wa Sheria.

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa baraza la Madiwani wa Halmashauri uliopitishwa na kufanyika tarehe 24/2/2017 mbele ya:-

ENG. GODFREY T. SANGA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mkalama*

JAMES J. MKWEGA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mkalama*

**L.S**

NAKUBALI,

Dodoma,
2 Novemba, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.)
*WN-OR-TAMISEMI*